## Je ni taarifa za aina gani zitakazokusanywa wakati wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022?

**Taarifa zitakazoulizwa zitahusu:-**

- Taarifa za kidemografia (umri, jinsi, hali ya ndoa)
- Taarifa za ulemavu (aina ya ulemavu, na chanzo cha ulemavu);
- Taarifa za uhamaji;
- Taarifa za vitambulisho vya utaifa na uhai wa wazazi;
- Taarifa za elimu;
- Taarifa za shughuli za kiuchumi;
- Taarifa za umiliki wa ardhi na TEHAMA;
- Taarifa za hali ya uzazi;
- Taarifa za vifo na vifo vitokanavyo na uzazi;
- Taarifa za nyumba, hali ya umiliki wa nyumba, vifaa/rasilimali na udhibiti wa mazingira;
- Taarifa za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu;
- Taarifa kuhusu mpango wa TASAF
- Taarifa za majengo/nyumba
- Anwani za makazi
- Taarifa za huduma za jamii katika ngazi ya Kitongoji/Shehia na Mtaa.

## Je ni taarifa za aina gani zitakazokusanywa wakati wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022?

**Ndio**, kama ambavyo hufanyika katika Sensa na tafiti nyingine za kitakwimu, kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Sura 351, taarifa utakazotoa kwa Karani wa Sensa zitakuwa **SIRI** na zitatumika kwa madhumuni ya kitakwimu pekee. Kwa mujibu wa sheria hii, kila Karani wa Sensa ata- saini kiapo cha kutunza siri za taarifa zote atakazokusanya na chini ya kiapo hicho hatakiwi kutoa taarifa alizotumwa kukusanya kwa mtu yeyote zaidi ya kuziwasilisha kama zilivyo katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar. Karani yeyote akithibitika kwenda kinyume na kiapo cha kutunza siri, atashitakiwa na kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria hii.

## Nitamtambuaje Karani wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022?

Karani wa Sensa atafika katika kaya akiwa na kitambulisho na sare maalum inayomtambulisha. Pia ataongozana na Mwenyekiti au Kiongozi wa Serikali ya Mtaa / Kitongoji/Shehia.

## Je, ni Wajibu Kisheria Kujibu Maswali ya Sensa?

Ndio, kujibu maswali ya Sensa ni matakwa ya kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Sura Namba 351. Kumbuka: Ushirikiano wako na Karani wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa kutoa taarifa sahihi ndio utakaorahisisha na kufanikisha Sensa ambapo matokeo yake yatachochea kasi ya maendeleo ya watu na makazi yao katika maeneo yote ya utawala nchini.

## Je, UVIKO-19 siyo kikwazo cha kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

Hapana, UVIKO-19 siyo kikwazo kwa yeyote kushiriki kwa nafasi yake katika Sensa ya mwaka 2022 kwani kulingana na maendeleo ya ugonjwa huu, Makarani na watendaji wote katika Sensa hii watazingatia tahadhari zote zinazoelekezwa na wataalamu wa afya ili kutokuwaambukiza wananchi au wao kuambukizwa na wananchi wakati wa zoezi la Sensa.

**Sensa kwa Maendeleo, Jiandae Kuhesabiwa**


**Ofisi ya Taifa ya Takwimu,**
Wizara ya Fedha na Mipango,
S.L.P. 2683, 18 Barabara ya Jakaya Kikwete,
Dodoma - TANZANIA

**Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali,**
Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango,
S.L.P. 2321, Mtaa wa Mazizini,
Zanzibar - TANZANIA


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

## SHIRIKI KIKAMILIFU

## SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022

## KWA MAENDELEO ENDELEVU YA TANZANIA

# SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022

Tanzania itafanya Sensa ya Watu na Makazi mwezi Agosti mwaka 2022 katika siku itakayotangazwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kabla ya zoezi la kuhesabu watu wote watakaolala ndani ya mipaka ya nchi usiku wa kuamkia Siku ya Sensa, shughuli mbalimbali za maandalizi hufanyika ambazo hujumuisha utoaji elimu kwa lengo la kuuelimisha umma juu ya umuhimu wa Sensa ili kuhakikisha kila mmoja anatambua umuhimu wa kuhesabiwa na kuhamasika kuhakikisha kwamba anahesabiwa na anahes- abiwa mara moja tu.

Elimu hii inajumuisha mada mbalimbali zikiwemo; Sensa ni nini, umuhimu wa Sensa, nani anapaswa kuhesabiwa, ni taarifa gani zitakusanywa wakati wa Sensa na umuhimu wa kuweka kumbukumbu za watu wote waliolala katika kaya usiku wa kuamkia Siku ya Sensa. Mambo muhimu unayopaswa kuyafahamu kuhusu Sensa ya Watu na Makazi ni yafuatayo:-

## Sensa ya Watu na Makazi ni Nini?

Sensa ya Watu na Makazi ni moja ya zoezi muhimu linalokusanya taarifa za kila mtu aliyelala ndani ya mipaka ya nchi usiku wa kuamkia siku ya Sensa. Sensa ya mwaka 2022 kama zilivyo Sensa zilizopita, itahusisha Makarani wa Sensa ambao watatembelea kaya zote nchini na kufanya mahojiano ya ana kwa ana baina ya Karani wa Sensa na Mkuu wa Kaya.

Ikiwa Mkuu wa Kaya hatakuwepo, Karani wa Sensa atafaya mahojiano na mtu mzima yeyote katika kaya ambaye ana taarifa za kutosha kuhusu kaya na wanakaya wenzake waliolala katika kaya husika usiku wa kuamkia Siku ya Sensa.

## Nini Lengo la Sensa ya Watu na Makazi?

Lengo la Sensa ya Watu na Makazi ni kupata taarifa sahihi za kidemografia, kijamii, kiuchumi na hali mazingira kwa lengo la kupata takwimu sahihi zitakazoiwezesha Serikali na wadau wengine kupanga kwa usahihi mipango ya maendeleo ya watu wake katika sekta mbalimbali za elimu, afya, hali ya ajira, miundombinu kama barabara, nishati na maji safi. Kwa msingi huo, Sensa ni zoezi muhimu ambalo kila mmoja kwa nafasi yake analazimika kushiriki na kutimiza wajibu wake ili kuhakikisha inakuwa ya mafanikio makubwa.

Hii itasaidia Serikali kutimiza wajibu wake kwa wananchi kulingana na idadi ya watu ya eneo husika ikiwa kama msingi mkubwa wa ugawaji ya keki ya taifa kwa kila eneo la utawala hapa nchini.

## Nani Anapaswa Kuhesabiwa?

Sensa ya mwaka 2022 kama zilivyo Sensa zilizopita, itafanyika nchi nzima na itahusisha watu wote watakaolala ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hii inamaanisha kuwa, watu wote watakaolala katika kaya binafsi usiku wa kuamkia Siku ya Sensa pamoja na watu wote watakaokuwa katika kaya za jumuiya kama vile hotelini, nyumba za kulala wageni, hospitalini, magereza, mabweni ya wanafunzi, kambi za jeshi, vituo vya kulelea watu wenye mahitaji maalum kama yatima na wazee, kambi za wavuvi, watu wasio na makazi maalum na vituo vya usafiri wa umma (kama vituo vya mabasi, garimoshi, viwanja vya ndege na bandari) watahesabiwa kwa kutumia utaratibu maalum utakaondaliwa na Kamati za Sensa katika ngazi ya mtaa, kitongoji na shehia

## Natakiwa kufanya nini wakati wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022?

Unachotakiwa kufanya ni kumpa ushirikiano wa kutosha Karani wa Sensa atakapokutembelea katika kaya kwa kujibu maswali yote atakayouliza kwa usahihi. Aidha, ukiulizwa swali na hujalielewa au hujasikia vizuri, unayo haki ya kumwomba Karani arudie kuuliza au kutoa ufafanuzi ili uweze kutoa jibu sahihi kulingana na swali lililoulizwa.

Ni muhimu kwa mkuu wa kaya kuhakikisha anachukua taarifa zote muhimu (kama umri, elimu, jinsi, hali ya ndoa, umiliki wa vitambulisho vya Taifa, shughuli za kiuchumi) za watu wote waliolala katika kaya yake usiku wa kuamkia Siku ya Sensa ili aweze kukumbuka wakati Karani atakakutembelea katika kaya.

## Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 itafanyika vipi?

Siku ya Sensa, Karani wa Sensa akiongozana na Mwenyekiti au kiongozi wa Serikali ya Mtaa au Kitongoji/Shehia atafika katika kaya akiwa na kitambulisho cha Karani wa Sensa na Dodoso la Sensa lililowekwa katika kifaa cha kielektroniki kiitwacho kishikwambi(Tablet) na kuuliza maswali ambayo yatajibiwa na Mkuu wa Kaya.

Ikiwa Mkuu wa Kaya atakuwa hayupo, mtu mwingine yeyote mzima katika kaya ambaye ana taarifa za kutosha kuhusiana na kaya na watu wote waliolala ndani ya kaya husika usiku wa kuamkia Siku ya Sensa anaweza kujibu maswali ya Sensa kwa niaba yake

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa